FUNZO LA 51

1. Yesu alikuwa na umri gani wakati alianza kufundisha Wayahudi?
-Alikuwa na umri wa miaka 30.

2. Ni Habari gani Njema ya Mungu ambayo Yesu alifundisha?
-Habari Njema ya Mungu ni kwamba ingawa dhambi zetu lazima ziadhibiwe na kifo, Mungu alikuwa anamtuma Mwokozi kutuokoa.

3. Mwokozi ambaye Mungu alikuwa anamtuma kuokoa watu ni nani?
-Yesu.

4. Yesu alimaanisha nini aliposema, "Wakati umefika, na ufalme wa Mungu umekaribia"?
-Yesu alimaanisha kwamba wakati umefika wa Mwokozi, na kwamba ufalme wa Mungu utashinda ufalme wa Shetani hivi karibuni.

5. Ni njia gani pekee ambayo mtu anaweza kumpendeza Mungu?
-Kwa kuamini Neno la Mungu.

6. Kwa nini Yesu aliwaita watu kuwa pamoja naye?
-Kwa sababu Yesu alitaka kuwafundisha ili waweze kuwafundisha watu wengine juu ya Mungu.

7. Walimu wa sheria walikuwa nani?



-Walikuwa Mafarisayo.

8. Ni jinsi gani mafundisho ya Yesu yalikuwa tofauti na mafundisho ya Mafarisayo?
-Kwa sababu Yesu alikuwa Mungu, Yesu alimjua Mungu Baba. Mafarisayo hawakumjua Mungu Baba.
-Kwa sababu Yesu alikuwa Mungu, Yesu alijua Neno la Mungu. Mafarisayo hawakujua Neno la Mungu.
-Kwa sababu Yesu alikuwa Mungu, Yesu aliamini Neno la Mungu. Mafarisayo hawakuamini Neno la Mungu.

9. Hapo mwanzo, mapepo walikuwa nani kabla ya kuwa mapepo?
-Mwanzoni, mapepo walikuwa malaika wazuri ambao Mungu aliwaumba hadi walipomfuata Shetani na kuwa wabaya.

10. Je, mapepo wanajua kuwa Yesu ni Mungu?
-Ndiyo.

11. Kwa nini mapepo yanamwogopa Yesu?
-Kwa sababu mapepo wanajua kwamba Yesu anaweza kuwatupa katika Ziwa la Moto wa Milele wakati wowote.

12. Ni jinsi gani dhambi inafanana na ukoma?
-Kama vile mtu huyo hakuweza kujiponya na ukoma, kwa hivyo sisi hatuwezi kujiponya wenyewe kutoka kwa dhambi.
-Kama vile hakuna mtu mwingine aliyeweza kumponya mtu huyo kutoka kwa ukoma, kwa hivyo hakuna mtu mwingine anayeweza kutuponya sisi kutoka kwa dhambi.
-Kama vile Yesu tu ndiye aliyeweza kumponya mtu huyo

kutoka kwa ukoma, ndivyo tu Yesu ndiye anayeweza kutuponya sisi kutoka kwa dhambi.

-Usiku mmoja mtu mmoja aliyeitwa Nikodemo alikuja kumtembelea Yesu.

Tusome Yohana 3:1-2

1-Basi palikuwa na mtu mmoja wa Mafarisayo, jina lake Nikodemo, mkuu wa Wayahudi.
2-Huyo alimjia usiku, akamwambia, Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.

-Wengi wa Mafarisayo walimchukia Yesu.
-Wengi wa Mafarisayo walisema kwamba nguvu za Yesu zilitoka kwa Shetani.

-Nikodemo alikuwa tofauti.
-Nikodemo hakumchukia Yesu.

-Nikodemo alitaka kuzungumza na Yesu na kumwuliza Yesu maswali mengi.

-Nikodemo alisema nini kwa Yesu?
-Nikodemo alisema kwamba alijua kwamba Mungu alimtuma Yesu.

-Nikodemo alijuaje kwamba Mungu alimtuma Yesu?



-Kwa sababu Yesu alikuwa akifanya miujiza mingi ambayo ni Mungu tu ndiye aliyeweza kufanya.

-Je Yesu alimjibu nini Nikodemo?

Tusome Yohana 3:3

3-Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.

-Yesu alisema kuwa hakuna mtu awezaye kuuona ufalme wa Mungu isipokuwa amezaliwa mara ya pili.

-Yesu alimaanisha nini?

-Yesu alikuwa na maana kwamba watu wote wamezaliwa chini ya ufalme wa Shetani, na kwamba lazima wazaliwe mara ya pili.

-Ni vipi watu wote wamezaliwa chini ya ufalme wa Shetani?

-Adamu na Hawa walipotenda dhambi na kutomtii Mungu, walitengwa kutoka kwa ufalme wa Mungu.

-Adamu na Hawa walipotenda dhambi na kutomtii Mungu, wakawa chini ya ufalme wa Shetani.

-Watoto wa Adam na Hawa, Kaini na Habili, walizaliwa chini ya ufalme wa Shetani.

-Kwa sababu Adamu na Hawa walitenda dhambi na kutomtii Mungu, watu wote walizaliwa chini ya ufalme wa Shetani.

-Yesu alikuwa na maana kwamba watu wote wamezaliwa chini ya ufalme wa Shetani, na kwamba lazima wazaliwe mara ya pili.
-Nikodemo alijibu nini?

Tusome Yohana 3:4

4-Nikodemo akamwambia, Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa?

-Nikodemo hakumuelewa Yesu.
-Nikodemo hakujua jinsi mtu anaweza kuzaliwa mara ya pili.

-Nikodemo alifikiri kwamba Yesu alikuwa anazungumza juu ya kuzaliwa mara ya pili kwa mwili.

-Je, Yesu alikuwa anazungumza juu ya kuzaliwa mara ya pili kwa mwili?
-La.
-Yesu alijibu nini?

Tusome Yohana 3:5

5-Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.



-Yesu alisema kwamba lazima tuzaliwe mara ya pili kwa maji na Roho.

-Kwanza, Yesu alisema kwamba lazima tuzaliwe kwa maji.

-Yesu alimaanisha nini “kuzaliwa kwa maji”?

-Je, “kuzaliwa kwa maji” kunamaanisha “kubatizwa”?
-La.
-Je, Yesu alimaanisha kwamba lazima tubatizwe ili kuzaliwa mara ya pili?
-La.

-Je, ubatizo unaweza kutuokoa?
-La.

-Yesu alimaanisha nini “kuzaliwa kwa maji”?

-Maji hufanya nini kwa uchafu?
-Inasafisha.

-Kama vile maji husafisha uchafu, vivyo hivyo watu wote lazima pia wasafishwe kwa dhambi.

-Yesu alimaanisha nini “kuzaliwa kwa maji”?

-Kuzaliwa kwa maji inamaanisha kwamba lazima tutubu dhambi zetu ili Mungu atusafishe dhambi zetu.

-Pili, Yesu alisema kwamba lazima tuzaliwe kwa Roho.

-Yesu alimaanisha nini “kuzaliwa kwa Roho”?

-Adamu na Hawa walipotenda dhambi na kutomtii Mungu, roho zao zilikufa kwa Mungu.

-Adamu na Hawa walipotenda dhambi na kutomtii Mungu, roho yao ambayo iliweza kujua, kupenda, na kutii Mungu ilikufa kwa Mungu.

-Kwa sababu roho yetu imekufa kwa Mungu, lazima Mungu atoe maisha mapya kwa roho zetu.

-Yesu alimaanisha nini “kuzaliwa kwa Roho”?

-Kuzaliwa kwa Roho inamaanisha kwamba Mungu Roho Mtakatifu lazima atoe maisha mapya kwa roho zetu.

-Kuzaliwa kwa maji inamaanisha kwamba lazima tutubu dhambi zetu ili Mungu atusafishe dhambi zetu.

-Kuzaliwa kwa Roho inamaanisha kwamba Mungu Roho Mtakatifu lazima atoe uzima mpya kwa roho zetu.

-Yesu alimwambia Nikodemo asishangae kwamba lazima azaliwe mara ya pili.

Tusome Yohana 3:7

7-Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili.



-Kwa nini Nikodemo hapaswi kushangaa kwamba lazima azaliwe mara ya pili?
-Hivi ndivyo Yesu alisema:

Tusome Yohana 3:6

6-Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho.

-Yesu alimaanisha nini, “Mwili huzaa mwili, lakini Roho huzaa roho?

-Yesu alikuwa na maana kwamba mwili unaweza kuzaa tu mwili.

-Yesu pia alimaanisha kwamba Mungu Roho Mtakatifu ndiye pekee anayeweza kuzaa roho ya mwanadamu.

-Kwa mujibu wa Mungu, kuna watu wawili tu ulimwenguni.

-Sio wazungu na watu weusi.
-Sio watu matajiri na watu masikini.

-Sio vijana na wazee.
-Sio wanaume na wanawake.

-Kwa mujibu wa Mungu, ni watu gani wawili tu duniani?

-Wale ambao wamezaliwa mara moja tu, na wale ambao wamezaliwa mara ya pili.

-Je, ni katika familia ya nani watu ambao wamezaliwa mara moja tu walipo?
-Wapo katika familia ya Shetani.

-Je, ni katika familia ya nani watu ambao wamezaliwa mara ya pili walipo?
-Wapo katika familia ya Mungu.

-Ni nini kingine Yesu alisema kwa Nikodemo?

Tusome Yohana 3:14-15

14-Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa;
15-ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye.

-Je, unakumbuka hadithi ya Musa na yule nyoka wa shaba jangwani?

-Kwa sababu Waisraeli walitenda dhambi na kutomtii Mungu, Mungu alituma nyoka wenye sumu kuwauma.

-Baada ya Waisraeli wengi kufa, Waisraeli ambao walikuwa bado wako hai walitubu.

-Kisha, Mungu alimwambia Musa atengeneze nyoka ya shaba, na aitundike juu ya mti.

-Mungu alisema kwamba ikiwa Waisraeli wangemwangalia



yule nyoka wa shaba, Mungu angewaponya.

-Je, Waisraeli waliweza kujiokoa kutoka kwa kifo?
-La.
-Ni nani pekee aliyeweza kuokoa Waisraeli kutoka kwa kifo?
-Mungu peke yake.

-Ni vipi Yesu na yule nyoka wa shaba ambaye Mungu alimwamuru Musa afanye jangwani wanafanana?

-Hivi ndivyo Yesu alisema:
-Kama vile nyoka wa shaba alikuwa ametundikwa juu ya mti, ndivyo Yesu pia angetundikwa juu.

-Kama vile Waisraeli waliokolewa walipomtazama yule nyoka wa shaba, ndivyo Yesu pia angewaokoa wale wanaomwamini.

-Ni nini kingine Yesu alisema kwa Nikodemo?

Tusome Yohana 3:16

16-Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

-Kwa sababu Mungu anawapenda watu wote, alimtuma Yesu Mwokozi.

-Kama tunamwamini Yesu, hatutakufa, lakini tutakuwa na uzima wa milele na Mungu.

-Ni nini kingine Yesu alisema kwa Nikodemo?

Tusome Yohana 3:17

17-Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye.

-Kwa nini Mungu alimtuma Yesu katika ulimwengu huu?

-Je, Mungu alimtuma Yesu atuhukumu?
-La.
-Je, Mungu alimtuma Yesu kutuangamiza?
-La.
-Kwa nini Mungu alimtuma Yesu katika ulimwengu huu?

-Mungu alimtuma Yesu kutuokoa kutoka kwa nguvu ya dhambi, mauti, na Shetani.

-Ni nini kingine Yesu alisema kwa Nikodemo?

Tusome Yohana 3:18

18-Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.

-Je, wale wanaomwamini Yesu watahukumiwa na Mungu?
-La.
-Je, wale ambao hawamwamini Yesu tayari wamehukumiwa na Mungu?



-Ndiyo.
-Kwa nini wale ambao hawamwamini Yesu tayari wamehukumiwa na Mungu?

-Kwa sababu hawaamini kwamba Yesu ni Mungu Mwokozi.

-Ni nini kingine Yesu alisema kwa Nikodemo?

Tusome Yohana 3:19-20

19-Na hii ndiyo hukumu; ya kuwa nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza kuliko nuru; kwa maana matendo yao yalikuwa maovu.
20-Maana kila mtu atendaye mabaya huichukia nuru, wala haji kwenye nuru, matendo yake yasije yakakemewa.

-Yesu alisema kuwa Yeye ndiye Nuru ambaye amekuja ulimwenguni.

-Yesu alisema kuwa watu waovu hawataki Nuru.
-Yesu alisema kuwa watu waovu wanataka kubaki gizani.

-Kwa nini watu waovu wanataka kubaki gizani?
-Kwa sababu wanapenda dhambi zao.

-Kwa nini watu hawataki kusikiliza Neno la Mungu?
-Kwa sababu wanapenda dhambi zao.

-Je, unataka kukaa gizani, au unataka kusikiliza Neno la Mungu?